# Utume Wa Kristo Ulimwenguni



Adrian Ebens

# Kwa Nini Yesu Alikuja Duniani?

Kuja kwa Yesu Kristo hapa duniani ilikuwa tendo la upendo,wema na rehema kupita ufahamu.Kushuka kutoka kwenye nafasi yake iliyoinuliwa na kuwa mwanadamu kunatujaza na mshangao. Kufikiria juu ya Mwana wa Mungu, ukuu wa Mbinguni akijinyenyekeza kuzaliwa katika hori la ng'ombe kama mtoto mchanga.

Athari za kitendo hiki peke yake zinapaswa kumeza kiburi cha asili cha wanadamu na tamaa.

Swali ambalo linapaswa kujibiwa ni kwanini alikuja? Je! Ni ujumbe gani muhimu ambao alikuja kutupatia? Sala ya Yesu, usiku kabla ya kusulubiwa kwake inatuambia wazi kusudi la utume wake. ´

> Nimekutukuza duniani. Nimemaliza kazi ambayo umenipa ifanye. Yohana 17: 4

Hapa Yesu anatuambia kazi ambayo Baba alimpa afanye. Kazi hii ilikuwa ya kumtukuza Baba. Utukufu wa Mungu ni nini? Musa aliuliza swali hili na Mungu akamfunulia Musa utukufu wake.

> Naye [Musa] akasema, "Tafadhali, nionyeshe utukufu wako." Kutoka 33:18
>
> ”BWANA akashuka ndani ya lile wingu, akasimama pamoja naye huko, **akalitangaza jina la BWANA**. BWANA akapita mbele yake, akatangaza, BWANA, BWANA, Mungu mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli; mwenye kuwaonea huruma watu elfu elfu, mwenye kusamehe uovu na makosa na dhambi; wala si mwenye kumhesabia mtu mwovu kuwa hana *hatia* kamwe; mwenye kuwapatiliza watoto

> uovu wa baba zao, na wana wa wana wao pia, hata kizazi cha tatu na cha nne. Kutoka 34:5-7

Kile alichokifunua Mungu ilikuwa ni tabia yake. Mwingi wa huruma, mwenye fadhili, si mwepesi wa hasira, mwingi wa rehema na kweli. Ni muhimu kiasi gani kujua mambo haya juu ya Baba yetu.  Kwa hivyo, tunaona kwamba Yesu alitufunulia tabia ya Baba yake.  Alituonyesha rehema, neema, uvumilivu, wema na ukweli wa Mungu.

Inamaanisha nini kwamba Mungu atawapatiliza uovu wa baba juu ya watoto hadi kizazi cha tatu na cha nne?Kwanza, hebu tuangalie kauli inayofanana na hiyo inayopatikana katika amri 10.

> ”Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu.” Kutoka 20:4-6

Mungu wa Biblia ni Mungu wa rehema. Wale wanaomwacha Mungu wa kweli na kuchagua mungu wa kisasi na mangamizi mwishowe watapata kile ambacho kwa upotovu walikiamini. Sio kwa sababu Mungu huwangamiza lakini kwa sababu wale wanaomwacha Mungu na kuondoka kwenye ulinzi Wake wanajiweka mikononi mwa mwangamizi, ambaye ni Shetani.

> ”Mfalme wao ni malaika kutoka kuzimu;  jina lake kwa Kiebrania ni Abadoni, na kwa Kiyunani, Apoliyoni - Mwangamizaji.”  Ufunuo 9:11

> ”Wala tusimjaribu Bwana, kama wengine wao walivyomjaribu, wakaharibiwa na nyoka. Wala msinung’unike,kama wengine wao

> walivyonung’unika, wakaharibiwa na mharabu(destroyer).”1 Wakorintho 10:9-10
>
> Shetani ndiye Mwangamizaji, lakini Kristo ndiye mrejeshaji. RH Novemba 26, 1895

Mungu huwatuma malaika zake kuwalinda na kuwakinga watoto wake. Wale wanaomkataa Mungu wa kweli, baada ya miaka ya maonyo na kusihiwa na Roho wa Mungu, mwishowe wanaachwa peke yao kulingana na uamuzi wao wenyewe. Hiki ndicho kilichotokea kwa Israeli katika uangamivu wa Yerusalemu baada ya taifa hilo kumkataa Masihi.

> ”Ee Yerusalemu, Yerusalemu, uwauaye manabii, na kuwapiga kwa mawe wale waliotumwa kwako! Ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja watoto wako, kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake chini ya mabawa yake, lakini hamkutaka! Angalieni, nyumba yenu mmeachiwa hali ya ukiwa.” Mathayo 23:37-38

# Hukumu za Mungu Hazitoki Moja Kwa Moja Kwake

Mungu hakuliangamiza taifa la Israeli. Aliacha taifa la Israeli liangamizwe na kufanywa ukiwa na mwangamizaji-shetani.

> "Wayahudi walikuwa wameghushi pingu zao wenyewe; walikuwa wamekijaza kikombe cha kisasi. Katika uharibifu uliowapata kama taifa, na katika ole zote zilizowafuata katika utawanyiko wao, walikuwa wakivuna tu mavuno ambayo mikono yao wenyewe ilikuwa imepanda. Nabii anasema: "Ee Israeli, umejiangamiza mwenyewe;""Kwa maana umeanguka kwa uovu wako." Hosea 13: 9; 14: 1. Mateso yao mara nyingi huwakilishwa kama adhabu

iliyopatilizwa juu yao na amri ya moja kwa moja ya Mungu. Ndio hivyo kwamba mdanganyifu mkubwa hutafuta kuficha kazi yake mwenyewe.Kwa kukataa kwa ukaidi upendo na huruma za kiungu, **Wayahudi walikuwa wamesababisha ulinzi wa Mungu kuondolewa kutoka kwao, na Shetani aliruhusiwa kuwatawala kulingana na mapenzi yake.** Ukatili wa kutisha uliotekelezwa katika uharibifu wa Yerusalemu ni dhihirisho la nguvu ya kisasi ya Shetani juu ya wale ambao wanakubali udhibiti wake". {GC 35.3}

Hivi ndivyo Mungu anavyomaanisha anapopatiliza uovu wa baba juu ya watoto hadi kizazi cha tatu na cha nne cha wale wanichukiao. Neno *kupatiliza* kwa Kiebrania linamaanisha *kuruhusu, kujali, kutekeleza, kukumbusha*. Baba yetu wa mbinguni anaruhusu maamuzi ya kila mtu kupata matokeo ya uchaguzi wake. Hawalazimishi watu wabadilishe mawazo yao. Anasimamia mchakato wa kila mtu kupokea matunda ya maamuzi yake wenyewe. Biblia inaelezea hivi.

”Msidanganyike, Mungu hadhihakiwi; kuwa kwa cho chote apandacho mtu, ndicho atakachovuna. Maana yeye apandaye kwa mwili wake, katika mwili wake atavuna uharibifu; bali yeye apandaye kwa Roho, katika Roho atavuna uzima wa milele.” Wagalatia 6:7-8

Mbegu za kiroho ambazo mtu hupanda zitaruhusiwa kuzaa matunda iwe kwa uzima wa milele au kwa kifo. Mungu anatekeleza mchakato huu kwa kumruhusu kila mtu kupata matunda ya maamuzi yake. Hili ndilo jambo pekee la haki awezalo kulifanya. Ingawa inasababisha maumivu na mateso makali sana kwa Baba yetu kuruhusu hili, Yeye hufanya hivyo kwa sababu Yeye ni mvumilivu na kwamba uhuru wa kuchagua umewekwa kwa wote.

"Nilionyeshwa kuwa hukumu za Mungu hazitatoka moja kwa moja kutoka kwa Bwana, lakini kwa njia hii: Wanajiweka wenyewe kando ya ulinzi Wake. Anaonya, kurekebisha, kukaripia, na kuonyesha njia pekee ya usalama; basi ikiwa wale ambao wamekuwa waangalizi

> Wake maalumu watafuata njia yao wenyewe bila Roho wa Mungu, baada ya maonyo ya mara kwa mara, ikiwa wanachagua njia yao wenyewe, basi Yeye huwaamuru malaika zake wasizuie mashambulio ya Shetani yaliyokusudiwa juu yao". {14MR 3}

Kuna wengine ambao wanasema kuwa nukuu hii kutoka kwa Ellen White sio kanuni ya jumla lakini inazungumzia tu tukio maalumu. Aya mbili kabla ya hiyo nukuu aliandika:

> ”Nilionyeshwa kuwa wakati ulikuwa karibu ambapo wale ambao Mungu alikuwa amewaonya na kuwakaripia na kuwapa nuru kuu lakini hawakuzisahihisha njia zao na kufuata nuru, angeondoa kutoka kwao ulinzi wa mbinguni ambao uliwahifadhi dhidi ya ukatili wa nguvu za kishetani; Bwana hakika angewaachia wao wenyewe kufuata hukumu na mashauri ya hekima yao wenyewe; wangeachwa peke yao, na ulinzi wa Mungu ungeondolewa kutoka kwao, na wasingelindwa na kazi za Shetani; kwamba hakuna hukumu na utabiri unaoweza kuwa na nguvu yoyote ya kupenya katika ulinzi ambao Mungu kupitia malaika zake ameuweka juu ya watoto wa wanadamu katika safari zao, katika nyumba zao wenyewe, katika kula na kunywa kwao. Popote walipo, jicho lake liko juu yao. Wamehifadhiwa kutoka katika hatari elfu, ambazo zote kwao hazionekani. Shetani ameweka mitego, lakini Bwana anafanya kazi kila wakati kuokoa watu wake kutoka kwenye hiyo mitego.” {14MR 2.3}

Hii ndiyo kanuni ambayo Mungu anaieleza katika Amri 10 na ni kanuni ambayo Yesu aliwaambia viongozi wa Kiyahudi akisema nyumba yao imeachwa ukiwa. Kanuni hii imesemwa tena kama kanuni ya jumla inayohusu mataifa yanayomkataa.

> ”Mungu anaendelea kuyavumilia mataifa. Hakuna shomoro anayeanguka chini bila yeye kujua. Wale wanaotenda mabaya kwa

> wenzao, wakisema, Je! Mungu anajuaje? siku moja watakutana na kisasi cha muda mrefu. Katika zama hizi dharau zaidi ya kawaida huonyeshwa kwa Mungu. Wanadamu wamefikia hatua ya dharau na kutotii ambayo inaonyesha kwamba kikombe chao cha uovu kimejaa kabisa. Wengi wamekaribia sana kikomo cha rehema. Hivi karibuni Mungu ataonyesha kwamba Yeye ndiye Mungu aliye hai. Atawaambia malaika, "Msimzuie tena Shetani katika harakati zake za kuangamiza. Na afanye ubaya wake juu ya watoto wa uasi; maana kikombe cha uovu wao kimejaa. Wameendelea kutoka kiwango kimoja cha uovu hadi kingine, wakiongeza kila siku uasi wao. Sitaingilia tena kuzuia mwangamizi asifanye kazi yake. " {RH, Septemba 17, 1901 par. 8}

Kwa hivyo wakati Ellen White anasema kile kitakachotokea katika siku za usoni, anaonyesha tu kwamba kanuni ya jumla ya kushughulikia uasi ilikuwa karibu kutendeka. Haikuwa tukio la mara moja. Hii inaunganishwa na kauli hizi za jumla (universal) juu ya malaika wa Mungu.

> **Malaika hutumwa kutoka nyua za mbinguni, sio kuja kuangamiza**, lakini kusimamia na kulinda roho zilizo hatarini, kuokoa waliopotea, kurudisha waliopotea kwenye zizi. {RH Mei 10, 1906}
>
> ”Malaika hawaji duniani kulaani na kuangamiza na kutawala, lakini ni wajumbe wa rehema kwa kushirikiana na Nahodha wa jeshi la Bwana, kushirikiana na mawakala wa kibinadamu ambao huenda kutafuta na kuokoa kondoo waliopotea. Malaika wameamriwa kupiga kambi karibu na wale wanaomcha na kumpenda Mungu.” {ST Novemba 20, 1893, par. 3}

Mshukuru Bwana kwa kuwa hawatumi malaika zake kuja kuangamiza. Yeye si muaji bali ni mhuishaji. Si mwangamizaji bali mrejeshaji.Wapendwa Mungu haui, hajawahi kuua wala hataua! Amri 10 ni Ufunuo wa jinsi alivyo. Yesu kristo alituonyesha jinsi Baba alivyo; Kwamba yeye Ni pendo, nuru na uzima. Shida ni sisi hatumwelewi.

> Ukweli huu utaeleweka kadri tunavyoendelea kujifunza. Kila kisa tutakielezea na mwisho tutazama katika penzi zito na Mungu Baba yetu.

## Mungu halamzimishi mtu yeyote

Ili kila mtu aweze kuwa na uhuru wa kuchagua na kupata matunda ya maamuzi yake mwenyewe, Mungu hawezi kumlazimisha mtu yeyote wakati wowote. Ukweli huu umeelezewa wazi katika Biblia na Roho ya Unabii.

> ”Nafsi yangu imo mkononi mwangu daima, Lakini sheria yako sikuisahau.” Zaburi 119:109

> Nanyi kama mkiona ni vibaya kumtumikia BWANA, **chagueni hivi leo mtakayemtumikia**; kwamba ni miungu ile ambayo baba zenu waliitumikia ng’ambo ya Mto, au kwamba ni miungu ya wale Waamori ambao mnakaa katika nchi yao; lakini mimi na nyumba yangu tutamtumikia BWANA. Yoshua 24:15

Pale mtu anapotishiwa kuuawa na yule ambaye anakataa kumfuata, huo sio uhuru wa kuchagua. Ikiwa Mungu anatishia kuwachoma moto na kuwaangamiza wale wanaokataa kumfuata, Basi ni kwamba hawapi uhuru wa kuchagua. Katika muktadha huu angekuwa analazimisha wamchague Yeye. Lakini serikali ya Mungu haiko hivyo.

> ”Utumiaji wa nguvu ni kinyume na kanuni za serikali ya Mungu; Yeye anatamani tu huduma ya upendo; na upendo hauwezi kulazimishwa; hauwezi kupatikana kwa nguvu au kwa mamlaka. Ni kwa pendo tu, upendo huamshwa. Kumjua Mungu ni kumpenda; Tabia yake lazima ionyeshwe tofauti na tabia ya Shetani.” {DA 22}

> ”Uasi haukupaswa kushindwa kwa kutumia nguvu. Nguvu ya kulazimisha inapatikana tu chini ya serikali ya Shetani. Kanuni za

> Bwana sio za utaratibu huu. Mamlaka yake imejikita juu ya wema, rehema, na upendo; na uwasilishaji wa kanuni hizi ndio njia ya kutumiwa. Serikali ya Mungu ina maadili, na ukweli na upendo vinapaswa kuwa nguvu anayotawala." {DA 759.1}

> "Nguvu ni suluhisho la mwisho la kila dini bandia." {ST Mei 6, 1897}

Ikiwa kanuni ya nguvu ni kinyume na serikali ya Mungu basi inawezekanaje kwa Mungu wakati wowote kutumia kanuni hizi? Roho ya unabii inaweka wazi kabisa kwamba nguvu inaweza kupatikana tu chini ya serikali ya Shetani.

> "Uwakilishaji potovu wa Shetani dhidi ya serikali ya Mungu, na utetezi wake wa wale waliomuunga mkono, yalikuwa madai ya kila mara dhidi ya Mungu. Manung'uniko na malalamiko yake hayakuwa na msingi; na bado Mungu alimruhusu atekeleze nadharia yake. **Mungu angeweza kumwangamiza Shetani na wote wanaomuunga mkono kwa urahisi kama mtu anavyoweza kuchukua kokoto na kuitupa chini. Lakini kwa kufanya hivyo angetoa mfano wa utumiaji wa nguvu. Nguvu zote za kulazimisha hupatikana tu chini ya serikali ya Shetani. Kanuni za Bwana sio za utaratibu huu. Asingefanya kazi kwenye msitali hu.** Asingekubali hata kidogo kwa mwanadamu yeyote kujiweka kama Mungu juu ya mwanadamu mwingine, akihisi kuwa na uhuru wa kumsababishia mateso ya mwili au akili. Kanuni hii kwa ujumla ni ya uumbaji wa Shetani." {RH, Septemba 7, 1897 par. 7}

Tunaambiwa kwamba Mungu angeweza kumuangamiza Shetani na wafuasi wake, lakini hili lingekuwa mfano wa matumizi ya nguvu. Hii inafafanua maana ya neno nguvu. Nguvu hujumuisha kumwangamiza mtu anayekupinga. Mungu hakuweza kufanya hivyo kwa sababu hii sio kanuni yake. Inamaanisha pia kwamba Mungu hangemuangamiza Shetani wakati wowote kwa sababu hii ingetoa mfano wa matumizi ya nguvu. Sikiliza wakati Ushuhuda wa Yesu ukiendelea na mada hii katika aya inayofuata.

”Kanuni za tabia ya Mungu zilikuwa msingi wa elimu inayowekwa kila wakati mbele ya malaika wa mbinguni. Kanuni hizi zilikuwa wema, rehema, na upendo. Nuru ya kujidhihirisha ilitakiwa kutambuliwa na kukubalika kwa uhuru na wote walioshika nafasi za uaminifu na nguvu. Lazima kukubali kanuni za Mungu, na, kwa njia ya kuwasilisha ukweli na haki, kuwasadikisha wote ambao walikuwa katika utumishi wake. Hii ilikuwa nguvu pekee ya kutumiwa. **Nguvu za kulazimisha hazikutakiwa kutumika kamwe**. Wote ambao walidhani kwamba msimamo wao umewapa nguvu ya kuwaamuru wenzao, na kudhibiti dhamiri, lazima wanyimwe nafasi zao; kwani huu sio mpango wa Mungu.” {RH, Septemba 7, 1897 par. 8}

Matumizi ya nguvu yaani kuwaangamiza wale wanaopinga ukweli hayahitajiki kabisa. Ni kwa upendo tu ndipo upendo huamshwa.

”Kanuni hizi zinapaswa kuwa msingi wa elimu katika kanisa la Mungu leo. Sheria alizozitoa zinapaswa kuzingatiwa na kuheshimiwa. Mungu ameamrisha jambo hili. Serikali yake ina maadili. **Hakuna kitu kinachopaswa kufanywa kwa kulazimishwa. Ukweli unapaswa kuwa nguvu iliyopo**. Huduma zote zinapaswa kufanywa kwa hiari, na kwa upendo wa Mungu. Wote ambao wameheshimiwa kwa kupewa nafasi za ushawishi wanapaswa kumwakilisha Mungu; kwa kuwa wakati wanapohudumu, huwa wako katika nafasi ya Mungu. Katika kila jambo walifanyalo matendo yao lazima yapatane na umuhimu wa nafasi zao. Kwa kadri nafasi zao zinavyokuwa za juu zaidi ndivyo kujitolea zaidi kunavyopaswa kudhihirishwa kwamba wanafaa kwa huduma hiyo. Kila moyo ambao unadhibitiwa na kanuni hizi utakuwa mwaminifu. Lakini wale wanaodai kuwa katika utumishi wa Mungu wanapokuwa watu wa lawama, huwa wanatumia kanuni za Shetani kumtoa Shetani; na hii haitafanya kazi kamwe.” {RH, Septemba 7, 1897 par. 9}

Je! Tunawezaje kuwafundisha watu kwamba ikiwa hawataamini kile tunachokiamini kwamba Mungu atawachoma na kuwaangamiza? Haya ni matumizi ya nguvu na huwa tunawalazimisha. Haiwezekani watu wa Mungu kufanya kazi katika mstari huu. Ukweli lazima uwe nguvu yetu iliyotawala. Ellen White anaendelea katika aya inayofuata...

> ”Katika mabaraza ya mbinguni iliamuliwa kwamba kanuni lazima zifanyiwe kazi bila kuharibu nguvu za Shetani hata mara moja; kwani lilikuwa kusudi la Mungu kuweka vitu juu ya msingi wa milele wa usalama. Muda lazima utolewe kwa Shetani kukuza kanuni ambazo zilikuwa msingi wa serikali yake. Ulimwengu wa mbinguni lazima uone kanuni zilizotekelezwa ambazo Shetani alitangaza kuwa zilikuwa bora kuliko kanuni za Mungu. **Utaratibu wa Mungu lazima utofautishwe na utaratibu wa Shetani. Kanuni mbaya za utawala wa Shetani lazima zifunuliwe.** Kanuni za haki zilizoonyeshwa katika sheria ya Mungu lazima zionyeshwe kuwa hazibadiliki, kamilifu, na za milele.” {RH, Septemba 7, 1897 par. 10}

Angalia nukuu isemavyo kwamba utaratibu wa Mungu lazima utofautishwe na utaratibu wa Shetani. Ellen White anaelezea jinsi utofauti huu ulivyokamilishwa wakati Yesu alipokuja duniani.

> ”Bwana alimruhusu Shetani kuendelea, na kuonyesha kanuni zake. Mungu alifunua kwamba kanuni zake zilikuwa sahihi, na alibeba walimwengu wasioanguka na ulimwengu wa mbinguni pamoja naye; lakini ilikuwa kwa gharama ya kutisha. Mwana wake wa pekee aliwekwa katika uwanja wa Shetani. **Bwana Yesu Kristo alifunua tabia iliyo kinyume kabisa na ile ya Shetani.** Wakati kuhani mkuu alipoweka kando mavazi yake maridadi, ya kifahari, na kuhudumu kwa mavazi meupe ya kitani ya kuhani wa kawaida, ndivyo Kristo alijitoa, na kuchukua umbo la mtumwa, na kutoa

> dhabihu, yeye mwenyewe kuhani na yeye mwenyewe kafara." {RH, Septemba 7, 1897 par. 12}

Ikiwa Shetani anawaua wale wanaompinga na Yesu akafunua tabia iliyo kinyume na Shetani basi inakuwa dhahiri kwamba Kristo hawaui wale wanaompinga na kwa hivyo Baba yake pia hawaui wanaompinga. Upendo hauwezi kulazimishwa. Biblia inasema pendo kamili huitupa hofu nje. Ikiwa Mungu anatishia watu kwa kifo basi Mungu hawezi kumwokoa mtu yeyote kutoka kwenye hofu/woga.

# Utume wa Kristo

Kwa uelewa ambao tumekwishapata, ningependa kuwasilisha kwako mkusanyiko wa nukuu kutoka kwenye Roho ya Unabii ambazo zinaonyesha wazi utume wa Kristo ulimwenguni. Kama ambavyo Yesu alisema, dhamira yake ilikuwa kufunua utukufu au tabia ya Baba. Katika Yohana 17, mistari 2 tu kutoka pale aliposema kwamba alikuja kumtukuza Baba, anasema hivi.

> "Jina lako nimewadhihirishia watu wale ulionipa katika ulimwengu; walikuwa wako, ukanipa mimi, na neno lako wamelishika." Yohana 17:6

Mungu alitangaza jina lake kwa Musa kama ilivyoonyeshwa katika Kutoka 34: 5. Hapa Kristo anatuambia kwamba Yeye hakutangaza tu bali kwamba alidhihirisha jina la Baba yake. Hiyo inamaanisha alituonyesha Baba. Kama alivyomwambia Filipo.

> "Yesu akamwambia, Mimi nimekuwapo pamoja nanyi siku hizi zote, wewe usinijue, Filipo? Aliyeniona mimi amemwona Baba; basi wewe wasemaje, Utuonyeshe Baba?" Yohana 14:9

Ninakuomba uzingatie kwa umakini nukuu zifuatazo ili kujua utume wa Kristo ulimwenguni ulikuwa ni upi.

> ”**Upendo** na **heshima** na ukamilifu **uliofunuliwa** katika **Injili** ni **ufunuo kwa mwanadamu wa tabia ya Mungu.** Haki na wema na fadhili ambazo zilionekana katika tabia ya Kristo zinapaswa kurudiwa katika maisha ya wale wanaokubali upendeleo wa Injili. Kwa kusoma neno, tunapaswa kumwona jinsi alivyo, na, tukipendezwa na mwonekano wa ukamilifu wake wa kimungu, tunapaswa kukua katika sura ile ile. **Tunapaswa kuelewa kwamba Injili inafunua utukufu wa Bwana kikamilifu. Ni kioo kinachofunua tabia ya Mungu kwa nafsi iliyoongoka. Mfano wa Mungu umefunuliwa katika tabia kamilifu ya Mwanawe,** ili tuweze kuelewa inamaanisha nini kufanywa katika sura ya Mungu, na kile tunachoweza kuwa ikiwa kwa kutazama kila wakati tutaruhusu tubadilishwe kutoka " utukufu hadi utukufu. ” {ST Februari 24, 1909, par. 3}

Injili imefunuliwa katika vitabu vinne vya kwanza vya Agano Jipya. Ni katika vitabu hivi ndipo utukufu kamili wa Bwana umefunuliwa. Hivi ndivyo Paulo anarejelea kama ifuatavyo:

> ”Lakini sisi sote, kwa uso usiotiwa utaji, tukiurudisha utukufu wa Bwana, kama vile katika kioo, tunabadilishwa tufanane na mfano uo huo, toka utukufu hata utukufu, kama vile kwa utukufu utokao kwa Bwana, aliye Roho.” 2 Wakorintho 3:18

Kristo anamwambia Filipo kwamba ikiwa anaweza kumwona Kristo anaweza kuona jinsi Baba alivyo.

> ”Katika Kristo Mungu aliona picha ya sura yake mwenyewe. Mungu alidhihirika katika mwili kwa sababu ya utambulisho mzima wa tabia yake katika tabia ya Kristo. Kwamba Mungu adhihirike hivi katika mwili ilikuwa ajabu kwa jeshi la mbinguni, "hata ile siri iliyokuwa imefichika tangu zamani na tangu vizazi vyote." {ST, Aprili 15, 1897 par. 10}

Tunaambiwa kwamba udhihirisho wa Kristo katika mwili ulifunua kabisa tabia ya Mungu.  Utambulisho mzima wa tabia yake ulifunuliwa wakati Kristo alipokuwa hapa duniani.

> ”Mungu anahitaji ukamilifu wa watoto wake. Sheria yake ni nakala ya tabia Yake mwenyewe, na ndio kiwango cha tabia zote. Kiwango hiki kisicho na mwisho kinawasilishwa kwa wote ili kusiwe na makosa kwa aina ya watu ambao Mungu atalazimika kuunda ufalme wake. **Maisha ya Kristo duniani yalikuwa udhihirisho kamili wa sheria ya Mungu**, na wakati wale wanaodai kuwa watoto wa Mungu watakapofanana na Kristo kitabia, watatii amri za Mungu.” {COL 315.1}

Ikiwa maisha ya Kristo duniani yalikuwa udhihirisho kamili wa sheria ya Mungu basi ni nini kingine Roho ya Unabii inachosema juu ya sheria ya Mungu?

> ”Sheria ya Mungu ni takatifu kama Mungu mwenyewe. Ni ufunuo wa mapenzi Yake, nakala ya tabia Yake, nakala ya upendo wa kiungu na hekima. {PP 52}

Ikiwa maisha ya Kristo duniani ni udhihirisho kamili wa sheria ya Mungu na sheria ni takatifu kama yeye mwenyewe na ni nakala ya tabia yake basi Kristo hapa duniani alifunua kabisa tabia ya Mungu.  Kwa uelewa huo, zingatia kauli hii yenye uvuvio:

> Kristo hakuwahi kumuua mtu yeyote ...{Ms62-1886.64}

Hivi ndivyo sheria ya Mungu inavyotuambia:

> Usiue.  Kutoka 20:13

Wacha tufuate mantiki.

1. Maisha ya Kristo duniani yalikuwa ni udhihirisho kamili wa sheria ya Mungu.
2. Kristo hakuwahi kumwua mtu yeyote.

3. Sheria inasema usiue.
4. Kwa hivyo, Mungu haui - mtu yeyote.

Hii ni rahisi kama vile ambavyo Biblia husema kuna Mungu Mmoja na Bwana Mmoja. Ulimwengu wa Kikristo hufanya ukweli huu rahisi kuwa mgumu sana lakini sivyo. Ni rahisi. Ulimwengu wa Kikristo pia hufanya wazo kwamba Mungu haui watu kuwa gumu sana wakati Kristo hakuua na Yeye ndiye ufunuo kamili wa Baba.

> ”Wale ambao wamepata baraka ya Mungu wanapaswa kuwa watu wenye shukrani zaidi. Wanapaswa kutoa kwa Mungu maneno ya shukrani kwa sababu Kristo alikuja katika sura ya mwili wenye dhambi, akivika uungu wake na ubinadamu, ili aweze kuleta mbele ya ulimwengu ukamilifu wa Mungu katika tabia yake mwenyewe. Alikuja kumwakilisha Mungu, sio kama hakimu mkali, bali kama baba mwenye upendo."Kwa maana Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele." Mungu ni upendo. Hii ilikuwa kweli kuu ambayo Kristo alikuja ulimwenguni kuifunua. **Shetani alikuwa amewasilisha vibaya tabia ya Mungu kwa ulimwengu, kwamba mwanadamu alisimama mbali na Mungu; lakini Kristo alikuja kuonyesha kwa ulimwengu sifa za Baba, kuwakilisha picha dhahiri ya nafsi yake.** "Kama vile Baba alivyonipa amri, ndivyo ninavyofanya.""Amri hii nimepokea kutoka kwa Baba yangu**."Lengo la utume wa Kristo kwa ulimwengu lilikuwa kumfunua Baba.**” {ST, Aprili 11, 1895 par. 2}

Kristo ndiye sura halisi ya nafsi ya Baba kama tunavyoambiwa katika Waebrania 1: 3. Ellen White anasema kwamba Kristo alikuja ulimwenguni kuonyesha sifa za Baba kama sura halisi ya nafsi ya Mungu.

> ”Lengo la utume wa Kristo kwa ulimwengu lilikuwa kumfunua Baba.” {ST, Aprili 11, 1895 par. 2}

Kauli hii ni udhihirisho kamili wa Yohana 17: 4. Utume wa Kristo ni kumfunua Baba. Asante Bwana kwa maneno haya ya wazi.

> ”Kristo aliinua tabia ya Mungu, akimpa sifa, na stahiki, kwa kusudi lote la utume wake mwenyewe hapa duniani, - kuwaweka sawa watu kupitia ufunuo wa Mungu. Katika Kristo neema ya baba na ukamilifu wa Baba viliwekwa dhahiri mbele ya watu. Katika sala yake kabla tu ya kusulubiwa, alitangaza, "Nimelidhihirisha jina lako." “Nimekutukuza duniani; Nimemaliza kazi uliyonipa kuifanya. Wakati lengo la utume wake lilipofikiwa, - ufunuo wa Mungu kwa ulimwengu, - Mwana wa Mungu alitangaza kwamba kazi yake imekamilika, na kwamba tabia ya Baba ilidhihirishwa kwa wanadamu.” {ST Januari 20, 1890, par. 9}

Kwa mara nyingine tena, tumeachwa bila shaka kuhusu kusudi la utume wa Kristo hapa duniani. Ilikuwa ni kuwaweka sawa watu kupitia ufunuo wa Mungu. Ufafanuzi wa Ellen White wa Yohana 17: 4 unaelezea vyema ujumbe wa Kristo:

> ”Pale lengo la utume wake lilipofikiwa, - ufunuo wa Mungu kwa ulimwengu, - Mwana wa Mungu alitangaza kwamba kazi yake imekamilika, na kwamba tabia ya Baba ilidhihirishwa kwa wanadamu.” {ST Januari 20, 1890, par. 9}

Inafurahisha sana kujua kwamba utume wa Kristo hapa duniani ulituonyesha jinsi Baba alivyo. Tunaweza kuwa na uhakika kwamba tunamjua Baba kupitia Yesu. Kwa hivyo, Kristo ndiye njia ya kwenda kwa Baba, ukweli wa Baba na uzima wa Baba.

> ”Lazima waziishi kanuni za mbinguni hapa duniani ikiwa wanataka kuwa washiriki wa familia ya kifalme mbinguni. **Maisha ya Kristo katika ulimwengu wetu yalipaswa kutoa uwakilishi katika tabia Yake mwenyewe ya ubora wa tabia ya Mungu.** Maneno Yake yalipaswa kutoa uhai, [kwamba] kwa maneno na matendo Yake ili wawe na dhana halisi ya tabia Yake. Wakristo kamwe hawapaswi

> kusahau kwamba wanapaswa kuwa wafuasi wa Kristo katika mambo yote.” {Ms11-1895.10}

Nukuu hizi haziwezi kuwa zimekosewa. Kwa nini watu husema kwamba Kristo alikuja tu kufunua rehema za Mungu hapa duniani lakini baadaye atafunua haki ya Mungu?  Hii ingeharibu ujasiri katika maandiko yaliyovuviwa ya Biblia na Roho ya Unabii.

> ”Pamoja na juhudi zao za kupinga kazi Yake, Kristo alikuwa akipata, hata huko Yerusalemu, ushawishi juu ya watu wengi kuliko wao. Umati wa watu ambao hawakupendezwa na mafundisho ya marabi walivutiwa na mafundisho Yake. Wangeweza kuelewa maneno Yake, na mioyo yao ilichangamka na kufarijiwa. **Alinena juu ya Mungu, sio kama hakimu anayelipiza kisasi, lakini kama baba mpole, na Akafunua sura ya Mungu kama inavyoonekana ndani yake.  Maneno yake yalikuwa kama mafuta kwa roho iliyojeruhiwa**. Kwa maneno Yake na kwa matendo Yake ya huruma Alikuwa akivunja nguvu za uonevu za mila za zamani na amri zilizotengenezwa na wanadamu, na akiwasilisha upendo wa Mungu katika utimilifu wake usiopimika.” {DA 204.4}

Ni jinsi gani ilivyoonyeshwa vizuri. Kristo alionyesha tabia ya Baba wakati alipokuwa hapa duniani.  Ulikuwa uwakilishi kamili.

> ”Ndivyo ilivyokuwa, na ndivyo itakavyokuwa hata mwisho wa wakati. Dhambi ni sifa ya Shetani, na kila wakati inaongozwa dhidi ya mema.  Roho ya Kaini ni dhahiri katika dini zote za uwongo.  **Kazi ya Shetani ni kulaani na kuangamiza, kuchukua uhuru wa mwanadamu na kuangamiza maisha yake.**  Makosa huwaongoza watu kutenda kama mawakala wa Shetani, kutekeleza malengo yake dhidi ya Mungu na haki. **Katika Nazareti Kristo alitangaza kwamba kazi Yake ilikuwa kurejesha na kuinua, kuleta amani na furaha.  Alikuja ulimwenguni kumwakilisha Baba, na akafunua**

> **nguvu Yake ya kimungu kwa kuwapa uhai wafu, kwa kuwarudisha wagonjwa na wanaoteseka kuwa sawa na wenye afya. <u>Alikuwa katika ulimwengu huu kama mti wa uzima</u>. Shetani anapigana na Kristo, Mrejeshaji wa kiungu. Mawakala wake wameshtakiwa dhidi ya kazi ya Mwokozi ya kumuinua na kumfanya mtu awe bora. Kifo cha kwanza katika ulimwengu wetu kilisababishwa na kazi ya kanuni za Shetani; na tangu wakati huo Kristo na wafuasi wake wamekuwa shabaha ya chuki yake mbaya.**” {ST Machi 21, 1900, par. 13-15}

Tofauti katika nukuu ziko wazi. Kazi ya Shetani ni kulaani na kuangamiza, kuchukua uhuru na kuangamiza maisha. Kazi ya Kristo ni kurejesha na kuinua na kuleta amani. Tofauti nzuri sana. Kwa kufanya kazi hii Kristo amemfunua Baba. Ninahisi furaha kama hiyo kusoma nukuu hizi. Natumaini wewe pia unafanya hivyo.

> ”**Kupitia kwa Yesu, Mwana wa Mungu, Baba amefunuliwa kikamilifu kwa ulimwengu**. Yesu aliwaambia wanafunzi wake: “Kama mngenijua mimi, mngemjua na Baba yangu pia; na tangu sasa mmemjua, na ninyi mmemwona. Filipo akamwambia, Bwana, tuonyeshe Baba, na inatutosha. Yesu akamwuliza, "Nimekaa pamoja nawe kwa muda mrefu, lakini hujanijua, Filipo? Yeye aliyeniona mimi amemwona Baba. ” Roho za maelfu zinalia leo, “Tuonyeshe Baba, nasi tutaridhika. Hatuwezi kudai Mungu kama Baba yetu hadi tutakapomwona. ” Yesu anasema kwa kila nafsi kama hiyo, kama vile alivyomwambia Filipo: “‘ Je! Nimekaa pamoja nawe kwa muda mrefu, na bado hujanifahamu? miujiza ambayo nimefanya kwa jina la Baba yangu, na bado hamjaelewa asili ya Mungu? **Nimeomba na wewe na kwa ajili yako, na bado hauwezi kuelewa kuwa mimi ndiye njia, ukweli, na uzima, na kwamba katika maisha yangu nimekufunulia tabia ya Baba yangu? Mimi ni mwangaza wa utukufu wa Baba yangu, mimi ni mfano dhahiri wa nafsi yake. ‘Huamini kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba yuko**

> **ndani yangu? maneno ninayosema kwako mimi siyazungumzi mimi mwenyewe; lakini Baba akaaye ndani yangu, ndiye azitendaye kazi hizo.** Niamini mimi kwamba mimi ni ndani ya Baba, na Baba ndani yangu; au sivyo niamini kwa sababu ya kazi zenyewe. Amin, amin, nawaambia, Yeye aniaminiye, kazi ninazofanya mimi atafanya yeye pia; na kazi kubwa kuliko hizi atafanya; kwa sababu mimi naenda kwa Baba yangu. '" {ST Juni 9, 1890, fungu la. 1}

Shida ileile ambayo Filipo alikuwa nayo, ipo leo. Hakuweza kuona kwamba Kristo alikuwa mwakilishi kamili wa Baba. Karibu ulimwengu wote wa Kikristo unateseka na upofu huo. Asante Bwana Yesu kwa kutuonyesha Baba ulipokuja ulimwenguni.

